SERIKALI> Imetoa takriban sh. bilioni 5.9 za kujenga minada mipya na kuk

# Ulega: Msomera ni mfano dhamira ya Dk. Samia kuendeleza wafugaji

NA MWANDISHI WETU

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imesema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amedhamiria kuwainua na kuwaendeleza wafugaji ndio maana serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha sekta ya mifugo, huku mfano ukiwa Kijiji cha Msomera.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alipofanya ziara ya kikazi ya siku moja katika Kijiji cha Msomera, kilichopo Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, kukagua maendeleo ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali inayowahusu wafugaji.

Miundombinu hiyo ni mabwawa ya maji, minada ya mifugo, majosho na malambo lengo likiwa kusogeza huduma karibu kwa wakazi wa kijiji hicho.

"Namshukuru na kumpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo serikali yake inahakikisha kila sekta inafikiwa katika maendeleo, wakiwemo wafugaji na wavuvi," alisema.

Alisema mbali na wafugaji ambao serikali imekuwa ikiwafikia kwa kuwapatia huduma mbalimbali za miundombinu kwa shughuli za mifugo, wavuvi na wafugaji wa samaki pia wanafikiwa.

"Hakuna lililosimama, yote yanasonga mbele wakandarasi waendelee kushirikisha vyema wenyeji ambao wanajua mazingira ya hapa (Msomera), na wenyeji kushirikiana na wakandarasi na wenyewe kuwashirikisha viongozi kila hatua," alisema.

Aliongeza kuwa, serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia katika mwaka huu imetenga fedha za ujenzi wa miundombinu ya maji kwa wafugaji, ikiwemo minada na kuwa takriban sh. bilioni 5.9 za kujenga minada mipya na kukarabati ya zamani na sh. bilioni 5.9 za kutengeneza majosho, zimetolewa.

### MKUU WA WILAYA

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Albert Msando, akitoa taarifa ya wilaya katika kikao cha Kijiji cha Msomera, ambacho Naibu Waziri Ulega alikuwa mgeni rasmi, alisema hadi sasa serikali imeshajenga majosho saba ya kuoshea mifugo, miradii ya malisho ya mifugo na kuwa maandalizi yamekamilika yakiwamo ya upatikanaji wa mbegu.

Msando aliongeza kuwa, idadi ya mifugo iliyopo katika kijiji hicho ni mingi kuliko idadi ya wakazi wake, ambayo ni zaidi ya 86,234 wakiwemo ng'ombe 28,049, mbuzi 32,743, kondoo 24,795 na punda 647.

### WANANCHI

Baadhi ya wanakijiji wa Msomera, katika kikao hicho walipata fursa ya kutoa maoni na kuuliza maswali kwa Naibu Waziri Ulega; na moja ya maoni yao ni kuomba vikundi vinavyojumuisha wanakijiji hao wapatiwe mashamba darasa na ng'ombe wa maziwa wafuge kisasa.

Naibu Waziri huyo katika kulifanyia kazi ombi hilo, aliielekeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), kufika katika kijiji hicho na kutoa elimu kuhusu mikopo kwa wafugaji hao, wafuge kwa tija na kibiashara kwa kuwa wana makazi ya kudumu.

Ulega yuko mkoani Tanga kwa ziara ya kikazi ya siku tatu, kujionea namna maendeleo ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya sekta za mifugo na uvuvi.

UTEKELEZAJI

tano tukazipeleka maabara ya Taifa na zikagundulika kwamba ni ugonjwa wa

kuwa, wanawake wano wengi wanajifungulia nyumbani badala ya vituo

udhaifu wa mwili, kikohozi, mafua pamoja na upele.

HABARI LEO UK 7.

# DC Kasilda hataki mitafaruku ya mifugo

**Na Mwandishi Wetu, Same**

MKUU wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Kasilda Mgeni ameliagiza Jeshi la Polisi wilayani humo kuwatafuta walipo wafugaji wanaodaiwa kuingiza mifugo kwenye mashamba ya watu na kuwajeruhi kwa kipigo wakulima watatu wa Kijiji cha Kisiwani-Barazani, Kata ya Kisiwani, wilayani humo.

Alitoa agizo hilo juzi wakati alipokwenda katika kijiji hicho ili kujionea athari zilizojitokeza baada ya wafugaji kuingiza mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima na kuwajeruhi wakulima watatu.

Kufuatia tukio hilo, aliagiza wafugaji wote ambao wameingia kinyemela bila kufuata taratibu za kisheria kuondoka mara moja kabla msako haujaanza na watakaobainika kukaidi agizo hilo sheria kali zitachukuliwa dhidi yao.

Kasilda aliwasihi pia wakazi wa kijiji



Kasilda Mgeni

hicho ambao wengi wao ni wakulima kuendelea kuwa watulivu wakati vyombo vya ulinzi na usalama vikiendelea na kazi yake na kuwa waache kujichukulia sheria mkononi kwa kutaka kulipiza kisasi.

Pia aliwataka watendaji na viongozi wa vijiji kusimamia sheria na kuacha tabia ya kuwapokea wafugaji wageni wanaoingia kinyemela bila kufuata taratibu za kisheria.

Alisema wafugaji wageni wanaoingia kinyemela katika wilaya hiyo mara nyingi wanaosababisha uvunjifu wa amani kwa kutoheshimu shughuli za watu wengine zinazofanyika ikiwemo kuingiza mifugo kwenye maeneo ya mashamba.

"Wote hapa mnafahamu mfugaji akitaka kutoka eneo moja kwenda sehemu nyingine lazima awe na barua kutoka uongozi wa serikali na anapotoka, kisha hiyo barua aipeleke kwenye kijiji anachotaka kuhamia na viongozi wa kijiji watajadiliana," alisema Mgeni.

Kwa upande wao wakulima wa kijiji hicho kwa nyakati tofauti walimweleza mkuu wa wilaya hiyo kuwa wamelazimika kufikisha kilio chao kwake kwa vile mara zote linapojitokeza jambo hilo hawapati msaada kutoka kwa viongozi wao wa serikali za vijiji.

Wakulima hao walidai mbele ya mkuu wa wilaya kuwa huenda viongozi wao wanahusika kuruhusu mifugo kuingizwa kwenye maeneo yao kwa vile wanapopeleka malalamiko yao hawawasaidii na taarifa hazifikishwi ofisi ya mkuu wa wilaya huenda kuna jambo linafichwa.

CamScanner

# Bil. 6.2/- kutumika ujenzi wa mabwawa kunyweshea mifugo

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema serikali imeridhia kutoa Sh. bilioni 6.2 kupitia bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya kunyweshea mifugo.

Ulega aliyasema hayo juzi wakati akiwa kwenye ziara ya kikazi ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa bwawa la maji la Kwekinkwembe lililoko wilayani Kilindi mkoani Tanga.

"Rais Samia Suluhu Hassan ameendelea kuboresha kila sekta, hakuna iliyoachwa nyuma, hivyo wafugaji watanufaika kwa kupata maji ya uhakika mara baada ya mradi wa ujenzi wa mabwawa ya kunyweshea mifugo maji kukamilika.

"Amegusa wakulima kwa kutoa mbegu za ruzuku, amegusa wafugaji mabwawa na majosho, hivyo hakuna aliyeachwa nyuma," alisema.

Ulega alimtaka mkandarasi anayefanya shughuli za ujenzi wa bwawa hilo , kuhakikisha anatoa taarifa ya kila hatua ya ujenzi na kuacha nakala wilayani hadi ngazi ya kijiji na kulikamilisha kwa wakati.

Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Abel Busalama aliwataka wananchi wa kijiji hicho kuhakikisha bwawa hilo linalojengwa kwa thamani ya Sh. milioni 504 na litakapokamilika lisimamiwe ili kuleta tija.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji nchini (CCWT) Wilaya ya Kilindi mkoani humo, Merieki Long'oni alishukuru namna serikali inavyowajali kwa kuwasogezea huduma ya maji karibu kwa ajili ya mifugo yao.